**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO**
**OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO**
S.L.P 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA.
Simu Na.: +255 (023) 2640006/7/8/9, Moja kwa moja: +255 (023) 2640015,
Barua pepe: vc@sua.ac.tz, Tovuti: https://www.sua.ac.tz

# TANGAZO LA AJIRA ZA MUDA 200 KUPITIA PROGRAMU MAALUM YA KUENDELEZA ZAO LA PAMBA NCHINI

**Utangulizi**
Chuo kikuu cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) kinashirikiana na Wizara ya Kilimo katika utekelezaji wa programu ya kushirikisha vijana katika kilimo ya Jenga Kesho Iliyo bora (Building a Better tomorrow-BBT). BBT inatekelezwa kupitia mikakati na miradi mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa mazao na baadhi ya malengo yake ni kuongeza ajira kwa vijana na wanawake 20,000 kupitia shughuli za kukuza ujuzi (internship), kuanzisha shughuli za kiuchumi 12,000 katika ngazi ya vijiji pamoja na kilimo cha mashamba makubwa (Block farms) ifikapo mwaka 2030.
Kama sehemu ya mkakati wa kuimarisha huduma za ugani hapa nchini, wizara ya kilimo imepanga kutekeleza pia program maalum ya huduma za ugani kupitia vijana wahitimu (BBT Agricultural Extension Entrepreneurship Scheme- BBT AEES). Kupitia BBT-AEES nafasi 200 zinahitajika kujazwa na wahitimu wa fani za kilimo kutoa huduma za ugani katika zao la pamba kwa utaratibu wa ajira za muda kama ifuatavyo:-

1. **Nafasi: Afisa kilimo/ (Nafasi 100)**
   ***Majukumu ya muhimu ni pamoja na:***
   a) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la pamba kwa kufanya yafuatayo:
      i. Kutoa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa wakulima kuanzia kuandaa shamba, kuvuna hadi kuhifadhi ghalani
      ii. Kutoa elimu na kusimamia ubora wa pamba kuanzia shambani hadi ghalani
      iii. Kufuatiliia na kuhakikisha kuwa wakulima wanazingatia kanuni za kilimo bora cha pamba
      iv. Kuandaa na kutoa taarifa ya kila wiki kuhusu maendeleao ya kilimo katika eneo husika
      v. Kuandaa mahitaji ya pembejeo kwa wakulima na kuyawasilisha katika mamlaka husika
      vi. Kusimamia na kuhakikisha pembejeo zinazopelekwa katika eneo husika zinawafikia wakulima kikamilifu

b) Kusajili wakulima na wadau wengine ikiwemo watoa huduma za pembejeo katika eneo lake kwenye mfumo wa kidijitali uliopo
c) Kutoa mafunzo na kuanzisha vikundi vya wakulima na kuvisimamia
d) Kuanzisha mashamba ya mfano na shamba darasa katika eneo la kazi
e) Kuwatambua wadau wa sekta kilimo waliopo katika eneo la kazi na kuwaunganisha na wakulima ili kupata huduma wanazotoa
f) Kuhakikisha kila mkulima ana daftari ambalo litatumika kujaza huduma zitakazotolewa na wadau mbalimbali
g) Kukusanya, kuandaa na kuchakata takwimu za uzalishaji katika eneo lake kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji takwimu (Agricultural Routine Data System (ARDS)
h) Kusimamia matumizi ya mfumo wa kidijitali ya kutoka huduma za ugani na
i) Kutoa ushauri kwa mazao mengine yanayolimwa na wakulima wa kijiji anachokisimamia

**Sifa zinazohitajika**

Kwa nafasi hii mwombaji awe na sifa zifuatazo:

i. Awe mtanzania mwaminifu, mweye kujituma na mahusiano mazuri na wengine
ii. Awe amehitimu shahada katika fani ya sayansi ya kilimo, au uzalishaji mazao kutoka chuo kinachotambulika na serikali
iii. Asiwe ameajiriwa au kufukuzwa kazi katika utumishi wa umma
iv. Awe hajawahi kufungwa kwa makossa yoyote ya jinai
v. Awe tayari kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya vijijini
vi. Awe na uwezo wa kufanya kazi vizuri bila kusimamiwa
vii. Awe tayari kufanya kazi kwa mkataba wa muda na kulipwa posho ya mwezi kama itakavyoainishwa katika mkataba
viii. Awe mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 40
ix. Awe tayari kusaini mkataba wa makubaliano wenye vigezo vya utendaji kazi kwa kipindi cha msimu husika
x. Uzoefu wa kazi katika zao la pamba au ushiriki wa mafunzo ya kukuza ujuzi (internship) ndani au nje ya nchi ni sifa za ziada

**2. Nafasi : Afisa kilimo msaidizi (Nafasi 70)**

***Majukumu ya muhimu ni pamoja na:***

a) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao la pamba kwa kufanya yafuatayo
   i. Kutoa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa wakulima kuanzia kuandaa shamba hadi kuvuna
   ii. Kutoa elimu na kusimamia ubora wa pamba kuanzia shambani hadi ghalani
   iii. Kufuatiliia na kuhakikisha kuwa wakulima wanazingatia kanunu za kilimo bora cha pamba
   iv. Kuandaa na kutoa taarifa ya kila wiki kuhusu maendeleao ya kilimo katika eneo husika

v. Kuandaa mahitaji ya pembejeo kwa wakulima na kuyawasilisha katika mamlaka husika
vi. Kusimamia na kuhakikisha pembejeo zinazopelekwa katika eneo husika zinawafikia wakulima kikamilifu

a) Kusajili wakulima na wadau wengine ikiwemo watoa huduma za pembejeo katika eneo lake kwenye mfumo wa kidijitali uliopo
b) Kushiriki katika kuanzisha mashamba ya mfano na shamba darasa katika eneo la kazi
c) Kuwatambua wadau wa sekta kilimo waliopo katika eneo la kazi na kuwaunganisha na wakulima ili kupata huduma wanazotoa
d) Kufuatilia na kusimamia utunzaji na usimamizi wa daftari la mkulima ambalo litatumika kujaza huduma zitakazotolewa na wadau mbalimbali
e) Kusaidia kukusanya, kuandaa na kuchakata takwimu za uzalishaji katika eneo lake kwa kutumia mfumo wa ukusanyaji takwimu (Agricultural Routine Data System (ARDS)
f) Kushiriki kusimamia matumizi ya mfumo wa kidijitali ya kutoka huduma za ugani

**Sifa zinazohitajika**

Kwa nafasi hii mwombaji awe na sifa zifuatazo:

i. Awe mtanzania mwaminifu, mweye kujituma na mahusiano mazuri na wengine
ii. Awe amehitimu stashahada katika fani ya sayansi ya kilimo au uzalishaji mazao kutoka chuo kinachotambulika na serikali
iii. Asiwe ameajiriwa au kufukuzwa kazi katika utumishi wa umma
iv. Awe hajawahi kufungwa kwa makossa yoyote ya jinai
v. Awe tayari kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya vijijini
vi. Awe na uwezo wa kufanya kazi vizuri bila kusimamiwa
vii. Awe tayari kufanya kazi kwa mkataba wa muda na kulipwa posho ya mwezi kama itakavyoainishwa katika mkataba
viii. Awe mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 40
ix. Awe tayari kusaini mkataba wa makubaliano wenye vigezo vya utendaji kazi kwa kipindi cha msimu husika
x. Uzoefu wa kazi katika zao la pamba au ushiriki wa mafunzo ya kukuza ujuzi (internship) ndani au nje ya nchi ni sifa za ziada

**3. Nafasi: Mhandisi kilimo/umwagiliaji (Nafasi 30)**

***Majukumu ya muhimu ni pamoja na:***

i) kutoa elimu ya utunzaji wa mashine pamoja na vifaa vinavyotumika katika uzalishaji mashambani
ii) Kusimamia uandaaji wa mashamba
iii) Kusimamia miundombinu ya umwagiliaji
iv) Kusimamia matengenezo na marekebisho ya mashine pamoja na vifaa vinavyotumika katika uzalishaji mashambani

v) Kusimamia utengenezaji na maboresho ya miundombinu ya shamba farm structures" (maghala, screen/green houses)
vi) Kusimamia utengenezaji na uboreshaji wa barabara mashambani
vii) Kusimamia uchakataji wa mazao yatakayozalishwa

**Sifa zinazohitajika**

Kwa nafasi hii mwombaji awe na sifa zifuatazo:

i. Awe mtanzania mwaminifu, mweye kujituma na mahusiano mazuri na wengine
ii. Awe amehitimu shahada ya uhandisi kilimo kutoka chuo kinachotambulika na serikali
iii. Asiwe ameajiriwa au kufukuzwa kazi katika utumishi wa umma
iv. Awe hajawahi kufungwa kwa makossa yoyote ya jinai
v. Awe tayari kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ya vijijini
vi. Awe na uwezo wa kufanya kazi vizuri bila kusimamiwa
vii. Awe tayari kufanya kazi kwa mkataba wa muda na kulipwa posho ya mwezi kama itakavyoainishwa katika mkataba
viii. Awe mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 40
ix. Awe tayari kusaini mkataba wa makubaliano wenye vigezo vya utendaji kazi kwa kipindi cha msimu husika
x. Uzoefu wa kazi katika zao la pamba au ushiriki wa mafunzo ya kukuza ujuzi (internship) ndani au nje ya nchi ni sifa za ziada

**Namna ya kutuma maombi**

Maombi yote yaambatane na

a) vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, NIDA, vyeti vya elimu ya sekondari na vyuo vya mafunzo ya kitaaluma.
b) Picha mbili za "passport size" za mwombaji za hivi karibuni
c) Wasifu (Curriculum vitae) wa mwombaji yenye anuani kamili, mawasiliano ya simu, barua pepe na anuani za wadhamini (referees) watatu wa kuaminika

Maombi yote yatumwe kwa Rasi wa ndaki ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo kupitia barua pepe coa@sua.ac.tz na nakala kwa mkuu wa idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia soil@sua.ac.tz. Waombaji wanashauriwa kutuma maombi yao kupitia barua pepe ingawa wanaweza pia kuleta maombi (nakala ngumu) moja kwa moja kwa ofisi ya Rasi wa Ndaki ya kilimo- SUA.

**Mwisho wa kutuma Maombi**

Maombi yote yawe yametufikia kabla au ifikapo tarehe 15 Disemba 2023.

Kwa maelezo zaidi au maswali juu ya tangazo hili tafadhali tupigie kupitia namba zifuatazo:
+255 657 796 719
+255 682, 308 890